# Muhtasari wa Matokeo ya Warsha ya Mtandao wa Wanawake iliyofanyika tarehe 12 Disemba 2023

***<u>Utangulizi:</u>*** *Warsha ya Mtandao wa Wanawake iliandaliwa pembezoni mwa kongamano la Jumuiya ya Afrika ya Tiba ya Maabara (African Society for Laboratory Medicine - ASLM) katika mji wa Cape Town nchini Afrika Kusini, tarehe 12 Disemba 2023. Lengo la Warsha hii ilikuwa kuanzisha Mtandao wa Wanawake kuhusiana na Mpango wa Kimataifa wa Kupunguza Vitisho vya Kibiolojia Barani Afrika. Warsha hii ilifanikishwa na wawakilishi kutoka Sekretarieti ya Shirikisho la kimataifa la vyama vya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi (International Federation of Biosafety Associations -IFBA) pamoja na Kamati ya uratibu wa Usawa kwa ufadhili kutoka kwa Serikali ya Kanada kupitia Mpango wake wa Kupunguza Tishio la Silaha. Malengo makuu ya warsha yalikuwa ni pamoja na kubainisha vipaumbele vya Mtandao, kuainisha washiriki na wadau wa Mtandao pamoja na muundo wake. Mkutano huu ulikuwa ni mwendelezo ya mikutano iliyofanyika awali kwa njia ya mtandao iliyoandaliwa na IFBA katika miezi ya Oktoba na Novemba 2023. Mikutano hiyo ya awali ililenga kusimamia umuhimu wa jinsia katika fani ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi, ikiweka msisitizo maalum kwenye bara la Afrika. Matokeo ya mikutano hiyo ya awali yamewasilishwa katika warsha ya moja kwa moja ili kujadili hatua zitakazoweza kuchukuliwa kwa ajili ya kuanzishwa kwa Mtandao na utekelezaji wa shughuli zilizopewa kipaumbele.*

**Kipaumbele cha 1: Utetezi kwa Ushiriki wa Wanawake katika shughuli za Usalama wa Afya Kikanda na Ulimwenguni kwa ujumla.**

*Agizo A: Utengenezaji wa Video mbalimbali katika Lugha rasmi za AU zinazooana na Muktadha wa Kiutamaduni wa Kiafrika.*

*Agizo B: Kuundwa kwa kundi la wanaume Watetezi wa Jinsia katika usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi.*

- Ufadhili ulipatikana kutengeneza video za uhamasishaji na kueneza uelewa kwenye usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi zilionyeshwa kwa washiriki. Hizi video zinategemea kusambazwa katika nchi mbalimbali Afrika na pia zitatafsiriwa katika lugha zote rasmi za Umoja wa nchi za Afrika (African Union – A.U.). Maoni yaliyokusanywa kutoka kwa washiriki yalijikita zaidi katika uundaji wa video kama sehemu ya utetezi inayolingana na miktadha ya kitamaduni ya hadhira inayolengwa ikiwa ni pamoja na: (a) kutumia viongozi kwenye jamii, wataalamu, au watu wengine mashuhuri kwenye jamii (kwa mfano, wanasiasa, wasanii n.k.); (b) ikiwa inalenga vijana, kwamba majukwaa mahususi yanayolenga vijana (kwa mfano Tiktok ) yatatumika ; (c) mbinu za uenezaji zilingane na muktadha wa pahala husika (k.m. kuongeza matumizi ya televisheni na redio badala ya mitandao ya kijamii pekee); na (d) video moja inaweza isitoshe kutimiza lengo kwa kuwa maeneo katika bara la Afrika yanatofautiana katika mahitaji ya uenezi.

International Federation of Biosafety Associations

In partnership with Canada

Global Partnership Against the Spread of Weapons and Materials of Mass Destruction

- Kwa ujumla kulikuwa na maafikiano kwamba pamoja na kuwa mtandao unalenga wanawake pia wanaume wanapaswa kushiriki na kuongeza nguvu katika juhudi za kukuza ushiriki wa wanawake katika eneo la usalama wa afya Afrika. Washiriki walijadili jukumu ambalo viongozi wa kiume watakayokuwa nalo katika kuajiri na kukuza fani za waajiriwa wa kike. Hoja zingine ziliangazia majukumu ya kijinsia ya kitamaduni nje ya mahali pa kazi yanayoathiri ushiriki wa wanawake, na kwamba mtandao unatakiwa kufikiria pia ni jinsi gani tunaweza kuwawezesha wanawake (haswa akina mama wenye watoto), ingawa majadiliano hayakuwa na mapendekezo ya jinsi wanaume wangeweza kushughulikia maswala haya.
- Kuna hitaji kubwa kuwajengea uelewa na ufahamu wataalamu na viongozi wa kiume kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia katika taaluma za usalama wa afya inayoendana moja kwa moja na taaluma pamoja na nguvu kazi, iwe zaidi ya kuunga tu mkono. Swala hili linahitajika kuwasilishwa na kusisitizwa kwa njia inayoonekana wazi kutoka kwa wanaume zinazoendana na miktadha ya kitamaduni yetu ya Kiafrika.

**Kipaumbele cha 1, Hatua Zinazofuata:**

- Kubainisha vipengele muhimu vya usanifu na ujumbe kwa ajili ya kutengeneza video kwa kuzingatia vipengele vya kitamaduni na lugha, ambayo itakayoweza kutumika vyema kwa walengwa katika eneo nzima:
- Kutoa tafsiri katika lugha zote rasmi za A.U., ikijumuisha tafsiri za video zilizoandaliwa awali;
- Kujadili zaidi nafasi ya wanaume kwenye utetezi wa kijinsia na juhudi za uhamasishaji kuhusu ujumuishaji wa jinsia kwenye maswala ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi katika bara la Afrika. Kupitia wanaume washiriki wa mtandao itengenezwe orodha ya mapendekezo kwa wataalamu na viongozi wa kiume ili kuwawezesha na kuhimiza ushiriki wa wataalamu wanawake katika usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi (hii inaweza kufanyika kwa kutumia zana ya utekelezaji ya IFBA DEI).

## Kipaumbele cha 2: Kuwawezesha Wanawake na Wasichana watakaoajiriwa na walioajiriwa kwenye kazi za Usalama wa Afya

*Agizo C: Kuwezesha upatikanaji wa elimu ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi kwa Wanawake na Wasichana*

*Agizo D: Ushauri na kuongeza kujulikana kwa Wanawake Watetezi wa usawa wa kijinsia katika usalama wa afya.*

- Kupata sifa na vyeti vinavyotambulika rasmi ambazo zinazoonyesha uelewa wa kiufundi na umahiri wa mtaalam ni muhimu hasa kwa wataalam wanawake wanapoingia na kushiriki kazini, kwani wanachukuliwa kwa uzito zaidi wanapokuwa na ushahidi wa aina hiyo.
- Uwepo wa programu za shahada ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi (kwa mfano iliyoanzishwa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro nchini Kenya) inatoa ujuzi muhimu kwa wasichana na wanawake waliopo na watakaoingia katika sekta ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi. Awali mafunzo rasmi ya shahada hayakuwepo yalikuwa yanatolewa tu kupitia kujengeana uwezo kwa kufundishana mtu mmoja mmoja kazini au uzoefu unajengwa kwa kufanya kazi kwa mfano, mawasiliano ya maswala yenye viashiria hatarishi (risk communication), ambayo ni fursa ambazo sio wakati wote zinajumuisha jinsia zote.
- Kuna kiwango cha juu cha motisha miongoni mwa wanawake wataalam wa usalama wa afya wa Kiafrika kutumia mafunzo na ushauri kutoka kwa wenzao kama zana za kukuza taaluma, hasa wakati mshauri akiwa ni mwanamke kutoka eneo lao na ana ujuzi kuhusu fursa na changamoto za ndani.

International Federation of Biosafety Associations

In partnership with Canada

Global Partnership Against the Spread of Weapons and Materials of Mass Destruction

**Kipaumbele cha 2, Hatua Zinazofuata:**

- Kusomesha wasichana katika shahada ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi nchini Kenya kwa kipindi cha miaka minne. Pia kuwashirikisha katika mipango ya usalama wa afya ya kimataifa ya kikanda na kimataifa.
- Kutambua na kutumia mbinu zilizopo ambazo zitaongeza kuonekana na kusikika kwa viongozi wanawake walioko kwenye usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi barani Afrika, na kuzingatia mapungufu yanayoweza kushughulikiwa moja kwa moja kupitia shughuli za Mtandao huu (kwa mfano, kuunda hifadhidata ya watetezi "champion" inayoweza kutumika kukuza elimu na kuongeza wigo la fursa za mtandao kwa wataalam wa kike chipukizi wa usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi) ;
- Kuainisha faida na fursa za kujiendeleza kitaaluma kwa wanawake na wasichana wa Kiafrika kwenye eneo hili ili kuweza kubainisha njia bora za uwekezaji. Je, mbinu kama vyeti vya kitaaluma, shahada za vyuo au mafunzo mtandaoni zinaleta manufaa tofauti kwa maendeleo ya kazi kwa wanawake wa Afrika kwa usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi?

## Kipaumbele cha 3: Kukuza Uongozi wa Wanawake wa Kiafrika katika usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi

*Agizo E: Mkusanyiko wa Hadithi za Mafanikio kutoka kwa Viongozi Wanawake wa Kiafrika katika usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi*

- Washiriki walijadili hitaji la kuhamasisha kuonekana na kusikika kwa viongozi wanawake wa Kiafrika katika sekta zote za usalama wa afya, sio tu kama njia ya kutoa motisha kwa wataalam wanaochipukia lakini pia kama hitaji muhimu la mitandao ya kitaaluma na wanawake hawa watumike kama washauri.
- • Kutoa nafasi kwa kuonekana na kusikika kwa wanawake watetezi "champions" ni kichocheo mojawapo cha kuhamasisha wanawake kujiongezea ufanisi cha kufuata fursa za uongozi na za kujiendeleza kitaaluma, hii inatokea iwapo wanahisi kazi yao inathaminiwa na sauti yao inasikika.
- • Ilisisitizwa kwamba ingawa msaada unaotolewa kwa wanawake wa safu ya uongozi katika usalama wa afya, inatakiwa kuzingatia tofauti za kijinsia katika kuainisha mahitaji ya kujengewa uwezo, hivyohivyo mbinu hazipaswi kulenga sana jinsia moja tu ili kuwapa nafasi ya kuendana na hali halisi ya dunia na aina tofauti za mahali pa kazi na miktadha ya kikanda.
- Majadiliano mengi kuhusu kupandishwa vyeo na kubaki katika sehemu ya ajira kwa viongozi wanawake wa Kiafrika yalielekeza jukumu la washirika wa wanaume katika kutetea ushiriki wao katika majukumu ya uongozi.

**Kipaumbele cha 3, Hatua Zitakazofuata:**

- Tambua wanawake wa Kiafrika katika uongozi wa usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi na kukusanya mitazamo yao katika ukuzaji wa taaluma na uhifadhi (ikiwa ni pamoja na changamoto na vikwazo vya kanda ya Afrika);
- Amua njia bora za uenezaji wa mitazamo ili kuwafikia walengwa wa Mtandao huu (kwa mfano wanawake ambao wako nje ya mtandao huu lakini ni wadau wa eneo hili, wafanya maamuzi na watunga sera).

International Federation of Biosafety Associations
In partnership with Canada
Global Partnership Against the Spread of Weapons and Materials of Mass Destruction

**Kipaumbele cha 4: Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Shughuli za Mtandao Zilizopewa Kipaumbele**

*Agizo F: Matumizi ya Zana ya Utekelezaji ya IFBA DEI kwa Shughuli za Mtandao na Usambazaji kwa Matumizi ya Jamii.*

- Zana ya Utekelezaji ya IFBA DEI ilitengenezwa ili kuwasaidia watoa maamuzi, watunga sera pamoja na uongozi wa juu wa Taasisi, kutathmini maendeleo yao katika kutekeleza vipengele vya utofauti, usawa, na ujumuisho (DEI) katika usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi.
- Zana iliyotengenezwa iliwasilishwa katika mikutano iliyofanyika kupitia mtandao na huu wa ana kwa ana ili kuwezesha kupima maendeleo na utekelezaji wa shughuli za Mtandao.

**<u>Kipaumbele cha 4, Hatua Zitakazofuata:</u>**

- Washiriki wapitie zana hii pamoja na maelezo mengine yanayopatikana kwenye tovuti ya IFBA. Kutakuwa na tukio la uenezaji wa zana hii itakayofanyika kwa njia ya mtandao mapema mwaka wa 2024;
- Mapitio ya pamoja ya Zana ya Utekelezaji ya DEI yatafanyika ili kuweka vipimo vya maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa kama kipaumbele cha Mtandao;
- Kutumia Zana ya Utekelezaji ya DEI ili kuchangia katika ushahidi kuhusu ujumuishaji endelevu wa kijinsia na upimaji wa maendeleo katika miktadha ya kiutamaduni ya kimataifa katika mazingira ya kitaalamu ya usalama na ulinzi wa vimelea hatarishi.

**Wadau na Washiriki wa Mtandao**

- Majadiliano kuhusu nani anayetakiwa kuwa sehemu ya Mtandao, wajumbe walikubaliana na kutoa dhana ya “kama mtu anaweza, anafaa ajiunge”. Washiriki wasiwe tu wanasayansi na wataalam wa maabara, lakini pia wajumuishe wataalam wengine katika jamii (kwa mfano, wataalamu wa ustawi wa jamii, viongozi wa kidini), wataalamu wa sera na sheria, na wawakilishi kutoka kwa uongozi wa juu (kwa mfano, wawakilishi wa nchi wanaohudhuria mikutano ya UNSCR1540 au BWC/Mikutano ya Kanuni “Codex” za FAO/mikutano ya WHO).
- Kutumia mitandao iliyopo katika sekta mbalimbali ni muhimu ili kuongeza wigo wa ufikiaji wa wadau na kuepuka kujirudia kwa juhudi, ikiwa ni pamoja na kutumia mifumo kama vile Afya Moja ili kutambua wadau katika sekta zote.
- Kuwasiliana na makundi mapya au bunifu haswa wale wanaohusika na sekta ya jinsia (kwa mfano, UN Women, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wa Afrika) ilionekana kuwa kipaumbele, kuwezesha uhamishaji wa maarifa na kazi shirikishi katika makutano ya jinsia na usalama wa afya.

International Federation of Biosafety Associations

In partnership with Canada

Global Partnership Against the Spread of Weapons and Materials of Mass Destruction

**Wadau na Washiriki wa Mtandao, Hatua Zinazofuata:**

- Kwa kuzingatia shughuli zilizopewa kipaumbele, washiriki wanatakiwa kukamilisha ufafanuzi na upeo wa washiriki na wadau ikiwa ni pamoja na kubainisha fursa za uangalizi na ushirikiano siku za mbele kutoka kanda zingine za ASEAN na LAC;
- Tambua mitandao ya kitaalamu ya kikanda na kimataifa iliyopo katika usalama wa afya, pamoja na mitandao ya kitaalamu inayokaribiana, inayoweza kutumika kutoa msaada katika kutekeleza shughuli zilizopewa kipaumbele za Mtandao huu;
- Kuainisha vikundi vya wadau vilivyopo na vinavyoweza kushirikishwa na Mtandao ili kubaini mbinu bora za ushirikishwaji au ushirikiano katika kutekeleza shughuli zilizopewa kipaumbele, ikijumuisha mapungufu ya kijiografia au kisekta.

***Muundo wa Mtandao***

- Uchanganuzi wa kikanda ulionekana kuwa muhimu, kwani kanda ndani ya bara la Afrika zina mahitaji tofauti, na mitandao tofauti itakoyoweza kutumika.
- Wazo la kuwa na Kamati ndogo za mada (subject matter subcommittees) za kikanda zilivutia wajumbe na zinaweza kuwa na manufaa kwa kuendeleza mafunzo na ushirikiano ya kikanda.

**Muundo wa Mtandao, Hatua Zinazofuata:**

- Kwa kuzingatia shughuli zilizopewa kipaumbele, itaandaliwa muundo rasmi wa Mtandao wa Wanawake ambao utasaidia utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa (ikiwa ni pamoja na malengo ya muda mfupi, wa kati na marefu), na kuruhusu ushiriki wa maana baina ya washiriki wote;
- Kuweka miongozo ya ushiriki wa wanaume katika Mtandao ikiangalia ni kiwango gani cha uwakilishi kitakachokuwa na manufaa kwa Mtandao mzima ;
- Kuunda kamati za masuala muhimu katika kanda tofauti , kubainisha wajumbe muhimu watakaoongoza hizi kamati katika kanda za Afrika.

***Hatua Zinazofuata baada ya Warsha:*** Mapema 2024, kutaundwa vikundi mbalimbali vya kazi ili kukamilisha muundo wa uendeshaji wa mtandao, pili kutambua na kuwashirikisha washiriki wa Mtandao, na tatu kutekeleza shughuli zilizopewa kipaumbele. Vikundi vya kazi vitazingatia uwakilishi wa kijiografia na usawa katika uwakilishi. Mwakilishi wa IFBA katika mawasiliano kwa kazi hii anaendelea kuwa Bi. Stephanie Norlock, Afisa Mwandamizi wa Programu ya IFBA (s.norlock@internationalbiosafety.org).

International Federation of Biosafety Associations

In partnership with Canada

Global Partnership Against the Spread of Weapons and Materials of Mass Destruction